# UCHUNGUZI NA MJADALA WA HALI YA ELIMU NA MAPENDEKEZO YA UBORESHAJI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA

## TAARIFA YA AWALI







Imeandaliwa na;

Dr. Zabron Kengera, Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Dar es Salaam

Dr. George Kahangwa, Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Dar es Salaam

Mr. Japhet Makongo, Mshauri Elekezi, Ubunifu Associates

**Vifupisho**

| | |
|---|---|
| AEK | Afisa Elimu Kata |
| BEST | Basic Education Statistics |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CSR | Corporate Social Responsibility |
| DAO | District Academic Officer |
| DED | District Executive Director |
| EK | Elimu ya Kujitegemea |
| MEWAKA | Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini |
| M&E | Monitoring and Evaluation |
| NGO | Non-Governmental Organisation |
| PCI | Project Concern International |
| SLO | Statistics and Logistics Officer |
| UWAWA | Umoja wa Walimu na Wazazi |
| VEO | Village Executive Officer |
| WASH | Water Sanitation and Hygiene |
| WEO | Ward Executive Officer |

**Shukrani**

Timu ya Wawezeshaji Dr Zabron Kengera (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), Dr George Kahangwa (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), Ndugu Japhet Makongo (Ubunifu Associate), Mwl. Livingstone Misana Gamba, Mwl. Alphonce Majura Kamela tunatoa shukrani nyingi kwa Serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma vijijini kwa kutuamini kuongoza na kuendesha zoezi hili la muhimu kwa niaba ya watu wa Musoma vijijini na wana Mara. Mapokezi, matunzo na ushirikiano mliotupatia yametuwezesha kufanya kazi yetu kwa ufanisi na hali kubwa. Kipekee sana tunammshukuru Mheshimiwa Mbunge Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, kwa kuasisi, kufadhili na kusimamia utekelezaji wa washa hii ya kipekee.

# Yaliyomo


Vifupisho ..... ii

Shukrani ..... iii

Yaliyomo ..... iv

1. Utangulizi ..... 1

   1.1. Usuli ..... 1

   1.2. Malengo ya Mjadala ..... 2

   1.3. Njia za Uendeshaji Mjadala na Uchambuzi ..... 2

2.0 Matokeo ya Mjadala na Uchunguzi ..... 5

   2.1 Mafanikio Yaliyopatikana ..... 5

   2.2 Changamoto zilizobainika ..... 6

   2.3 Chanzo na vichocheo vya changamoto ..... 7

3.0 Mapendekezo na njia za kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kuinua ufaulu. ..... 10

   3.1 Kuandaa na kutumia Ramani ya Mabadilliko (*Roadmap to Change*) ..... 10

   3.2 Mapendekezo ya Hatua za Utekelezaji ..... 10

4.0 Hitimisho na Maoni ya Wawezeshaji ..... 16

   4.1 Kupitia Mjadala washiriki wamepata kujifunza yafuatayo ..... 16

   4.2 Hitimisho na Mafunzo Makuu yaliyotokana na Mjadala: ..... 16

   4.3 Maoni ya timu ya wawezeshaji ..... 17

Rejea ..... 19

Viambatisho ..... 20

# 1. Utangulizi

## 1.1. Usuli

Ofisi ya Mbunge wa jimbo la Musoma Vjijini kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Musoma iliandaa mjadala wa pamoja wa hali halisi ya utoaji wa elimu ya msingi na sekondari katika Halmashauri ya Musoma, na kutoa mapendekezo ya kuboresha ufaulu. Lengo kuu la mjadala huu lilikuwa kufanya uchambuzi wa kina wa mambo yanayoathiri ujifunzaji na ufafaulu wa wanafunzi wa shule za msimgi na sekondari za Musoma na kutoa mapendekezo ya kuboresha matokeo ya elimu.

Mjadala huu ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wa elimu na kwa uwakilishi wa nafasi zao. Hawa ni pamoja na walimu wa taaluma 120 wa shule za msingi, Maafisa Elimu Kata 21, Walimu wakuu wa shule za ssingi 120 na Wakuu wa shule za sekondari 46 katika Halmshauri ya Musoma. Wengine ni Maafisa watendaji wa Kata 21 na Madiwani 21. Aidha, viongozi mbalimbali waandamizi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiongoza na Mkuu wa Wilaya ya Musoma walihudhuria kwenye mrejesho na majumuisho.

Mjadala huu ni sehemu ya mwendelezo wa juhudi za uongozi wa Mkoa wa Mara kuchambua changamoto zinazoikabili sekta ya elimu na kutafuta njia za kuzitatua kwa lengo la kuinua kiwango cha uafaulu wa wanafunzi kwa viwango vya kitaifa. Awali, ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliandaa kongamano la wadau wa elimu mwaka 2019 na kujadili changamoto zilizosababisha matokeo hafifu kwa shule za msingi na sekondari. Aidha Mwaka 2023, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini aliandaa Mkutano wa Wakuu wa shule za sekondari za Jimbo la Musoma kwa lengo kama hilo. Mjadala huu, pamoja na vikao vingine vya wadau kujadili suala la elimu vimechochea mabadiliko na kuongezeka kwa ufaulu wa mitihani ya kitaifa kwa kiasi fulani. Serikali na wadau wameendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto zinazojitokeza. Hii ni pamoja na kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu, kama vile kujenga shule mpya, kuongeza madarasa, maabara, maktaba, vyoo na nyumba za walimu. Serikali na wadau wa elimu wanaendelea kutoa vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia hususani kwa masomo ya sayansi, kwa hatua. Aidha idara ya elimu sekondari na ya msingi zimeendelea kuratibu

mafunzo ya walimu kazini na kutoa motisha stahiki kwa walimu kulingana na uwezo wa kibajeti (kwa bajeti ya serikali).

Taarifa ya Afisa elimu msingi inaonesha kuwa, juhudi zilizofanyika zimeonesha mabadiliko kidogo kwenye ufaulu wawanafunzi kwa mwaka 2024. Katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi, idadi ya watahiniwa waliofaulu kwa kupata daraja la A imeongezeka kutoka watahiniwa 17 mwaka 2023 hadi watahiniwa 138 mwaka 2024.

Hata hivyo, Taarifa ya Afisa ya Elimu ya awali na msingi, kuhusu matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2024 imeonyesha kuwa kiwango cha ufaulu wa jumla kimeshuka kwa asilimia 2.49% kutoka asilimia 75.23% mwaka 2023 hadi asilimia 72.74% mwaka 2024. Aidha imedhihirika pia kuwa kiwango cha ufaulu, hususan kwa shule zinazomilikiwa na serikali siyo cha kuridhisha ukilinganisha na shule chache zinazomilikiwa na taasisi binafsi. Kwa elimu ya sekondari kiwango kimepanda kwa asilimia 12.89% kutoka asilimia 72.42% mwaka 2023 hadi asilimia 85.31% mwaka 2024.

### 1.2. Malengo ya Mjadala

Mjadala huu uliongozwa na malengo yafuatayo;

a) Kujadili kwa uwazi kiini cha changamoto na vikwazo vinavyoathiri uelewa na uafaulu wa wanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari
b) Kupendekeza mikakati ya uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa wadau wa elimu katika ngazi na kada mbalimbali
c) Kujifunza na kubadilishana uzoefu wa njia zenye ufanisi za kujenga uwezo wa wadau wa elimu kuinua kiwango na ubora wa elimu wilayani

### 1.3. Njia za Uendeshaji Mjadala na Uchambuzi

Mjadala na uchambuzi vilifanyika kwa njia zifuatazo.

a) Kurejea na kuchambua taarifa na takwimu mbalimbali:

Zoezi hili lililenga kupata uhalisia kuhusu hali ya elimu, hususani sababu zinazochangia kuongezeka au kupungua kwa ufaulu wa wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari katika wilaya ya Musoma. Miongoni mwa taarifa zilizochambuliwa ni pamoja na

- Taarifa za idara ya elimu kuhusu utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka
- Muhtasari wa mijadaa ya wadau wa elimu mkoani Mara (Mjadala wa Mkoa 2019 na kikao cha wakuu wa sekondari 2023)
- Takwimu mbalimbali za elimu zinazotolewa kila mwaka na Wizara Elimu, Sayansi na Tekinolojia (Basic Education Statistics-BEST)

b) Majadiliano na wadau wa elimu

Kwa muda wa siku tatu mfululizo, Wataalamu wawezeshaji walipata fursa ya kukutana na makundi mbalimbali ya wadau ya elimu, yaani walimu wa Taaluma Shule za msingi na sekondari, Maafisa Elimu Kata, Watendaji wa Kata, Walimu wakuu wa shule za msingi na Wakuu wa shule za sekondari. Wengine ni Madiwani na Maafisa waandamizi wa serikali kutoka Idara za elimu na sekta zingine kutoka ofisi za Halmashauri.

c) Kazi za vikundi

Vikundi vya wadau vilitumia jedwari la uchambuzi wa hali ya utendaji wa kila shule kwa kutumia vigezo vinavyohusu masuala yaliyojadiliwa (angalia kiambatisho A). Aidha, vikundi vingine vilitumia jedwari la kutengeneza njia ya mabadiliko (Kiambatisho B), yaani namna ya kuboresha elimu katika kila shule.

d) Mrejesho wa matokeo ya uchambuzi na majadiliano kwa uongozi ngazi ya Wilaya

Katika siku ya tatu ya mjadala tajwa, kilifanyika kikao kwa nia ya kutoa mrejesho wa kilichojadiliwa na kukubaliwa na wadau mbalimbali wa elimu. Kikao hicho kiliwahusisha Viongozi waandamizi wa wilaya (Mkuu wa Wilaya, Afisa Tawala, Mkurugenzi Mtendaji, na Maafisa wa halmashauri, Mbunge na Madiwani. Wengine ni maafisa Watendaji wa kata zote, maafisa elimu wa kata, walimu wakuu shule za msingi na Wakuu wa Sekondari.

**Jedwali 1: Mahudhurio ya mrejesho wa matokeo ya mjadala wa hali ya Elimu katika Halmashauri ya Musoma**

| | **Wajumbe** | **Idadi** |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Musoma | 2 |
| 2 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma | 1 |
| 3 | Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini | 2 |
| 4 | Viongozi waandamizi wa Chama Cha Mapinduzi | 1 |
| 5 | Madiwani | 21 |
| 6 | Maafisa Watendaji wa Kata | 21 |
| 7 | Maafisa Elimu wa Kata | 21 |
| 8 | Walimu wakuu wa Shule za Msingi | 120 |
| 9 | Wakuu wa Shule za Sekondari | 28 |

## 2.0 Matokeo ya Mjadala na Uchambuzi

Mjadala wa siku tatu umebainisha masuala kadhaa yanayoathiri pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa mipango ya kuboresha elimu kwenye Halmashauri ya Musoma. Kwa ujumla, mjadala, ulibaini uwepo wa maendeleo kiasi katika elimu, ambapo kuna maeneo kadhaa yanayoonyesha kuongezeka kwa ubora wa elimu ngazi ya msingi na sekondari. Vilevile mjadala ulithibitisha kuwa kuna changamoto zinazokwamisha ujifunzaji wa wanafunzi na ufaulu, na kwamba ni zile zile zilizokwisha ibuliwa katika tathmini na uchambuzi uliotangulia. Changamoto hizi zinapelekea kupungua kwa viwango vya ufahamu wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari.

## 2.1 Mafanikio Yaliyopatikana

Imebainika kuwa, walimu kwa kushirikiana na viongozi wa kata (Diwani, Watendaji wa kata) na watendaji wa vijiji wameendelea kushughulikia masuala mbalimbali na kusaidia sekta ya elimu kupiga hatua. Hayo yamedhihirika katika;

a) Kuongezeka kwa ubora wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya, ujenzi wa miundombinu kama vile madarasa, maabara, maktaba; Ongezeko la vifaa na nyenzo za kujifunzia kama vile vitabu, nk;
b) Kuongezeka kwa ufaulu ( katika matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 12.89% kutoka asilimia 72.42% mwaka 2023 hadi asilimia 85.31% mwaka 2024).
c) Ongezeko la upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi na hamasa ya uchangiaji chakula hicho katika baadhi ya kata, kama vile Mugano, Bukwaya, na Muhoji;
d) Upatikanaji wa walimu tarajali na wa kujitolea (mfano katika Kata ya Mugango, shule ya sekondari Mugango ilikuwa na walimu 5 wa kujitolea lakini pia ilipokea walimu 11 tarajali kutoka UDSM – 7 na UDOM – 4);
e) Kuongezeka kwa mahusiano mazuri kati ya shule na jamii katika baadhi ya maeneo.

### 2.2 Changamoto zilizobainika

Mjadala na uchambuzi umebaini uwepo wa changamoto nyingi zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kuleta tija zaidi. Changamoto zimegawanyika katika makundi makuu matatu; yaani changamoto zilizoko shuleni (zinachangia 40%), changamoto zilizoko katika jamii (zinachangia takriban 25%) na changamoto zilizoko katika ofisi na taasisi zenye mamlaka (mchango wake ni takribani 35%). Ufafanuzi wa changamoto hizi kama inavyooneshwa hapa chini;

a) Changamoto ngazi ya shule
- Baadhi ya wanafunzi hawana hamasa ya elimu,
- Uwepo wa utoro na mahudhurio hafifu ya wanafunzi,
- Kupungua kwa ari ya wanafunzi kusoma/kujifunza,
- Nidhamu ya wanafunzi isiyoridhisha,
- Uwiano mkubwa wa wanafunzi na walimu (*Pupil-Teacher ratio*). Uwiano wa kijinsia, msawazo wa ikama, na walimu kuhama au kuhamishwa kituo baada ya muda mfupi,
- Motisha ya kufundisha iko chini na kutokuwepo ari na kujituma,
- Ujuzi/weledi duni wa mbinu za kufundishia zenye tija,
- Miundombinu na mazingira ya kujifunza na kufundishia (Msongamano wa wanafunzi darasani, nyumba za walimu, Ofisi, Maktaba, Maabara, iwanja vya michezo na burudani na majina huduma ya Afya (WASH),
- Ukosefu wa umeme katika baadhi ya shule. Ilibainika kwa mfano, kwamba shule 22 za msingi hazijaunganishwa na umeme (angalia kiambatisho C)
- Huduma saidizi zisizotosheleza, kama vile kutopatikana kwa chakula na lishe kwa wanafunzi. Ilibainika kuwa, Wanafunzi wengi hususan shule za msingi hawapati chakula shuleni. Baadhi ya kaya hazina chakula cha kutosha nyumbani. Chakula kinachotolewa hakina virutubisho muhimu. Shule zenye chakula zinamudu kutoka uji au makande. Baadhi ya shule (kwa mfano Mugango, Bukwaya, na Muhoji) zinajitahidi kutoa chakula lakini hakikidhi

ubora wa viwango vinayotakiwa kwa mwanafunzi. Vilevile kuna ukosefu wa Ushauri nasaha, pamoja na mpango wa maji salama, afya (WASH, nk.)

**b) Changamoto au masuala yanayohusu wazazi na jamii**

- Kuna utayari usioridhisha na ushiriki hafifu kwa baadhi ya wazazi na jamii, unaojionesha kupitiakutotoa huduma muhimu kwa wanafunzi kama vile mavazi, vifaa vya shule, chakula, michango ya kuinua taaluma)
- Kuna maelewano/ushirikiano dhaifu katika baadhi ya maeneo, baina ya wazazi, walimu, viongozi wa jamii, na mamlaka za usimamizi wa elimu

**c) Masuala yanayohusu taasisi na ofisi zenye mamlaka juu ya elimu (Ngazi ya Kijiji, Kata na Halmashauri)**

- Hadi sasa kuajiri/kupanga walimu hakujaweza kukidhi mahitaji halisi, hivyo kuna upungufu mkubwa wa walimu
- Kuna mgawanyo/mtawanyo mbaya wa walimu kwenye shule. Baadhi ya shule zina walimu wengi kuliko mahitaji ya kawaida wakati baadhi ya shule zina upungufu mkubwa
- Kiasi/kiwango cha usaidizi kinachotolewa kwa shule, kama vile fedha, vifaa, na nyenzo ni kidogo; yaani hakitoshelezi mahitaji.
- Kutofanyika kwa ufuatiliaji na tathmini (M&E), na kutotolewa kwa mrejesho wa karibu na wenye tija.
- Kutokuchukua hatua za kuthibiti maovu yaliyoibuliwa na kutolewa taarifa kwa mamlaka za juu.

## 2.3 Chanzo na vichocheo vya changamoto zilizopo

Mjadala ulibainisha kuwa zipo sababu zinazochochea changamoto zilizotajwa. Kwa maoni ya washiriki wa mjadala, sababu zinazohisiwa zimegawanyika katika maeneo manne (4);

a) **Uongozi, utawala, usimamizi na uthibiti**

- Maamuzi yenye ushiriki na ushirikishwaji dhaifu katika ngazi ya kijiji, kamati za shule/bodi, uongozi wa shule. Ilibainishwa kuwa, baadhi ya vikao vinatawaliwa na maagizo/maelekezo na hata vitisho badala ya mashauriano.
- Uteuzi wa nafasi za uongozi usiyozingatia taratibu/miongozo na weledi. Mathalan, badala ya kuteuliwa mwalimu mahiri wa somo anateuliwa mwalimu mhairi wa mwalimu mkuu/kiongozi.
- Uhamisho kwa walimu usiozingatia taratibu. Walimu toka nje ya Mkoa wa Mara wanaitumia Halmashauri kama kiingilo cha ajira na baada ya kuthibitishwa kazini wanahama.
- Kukosekana kwa motisha kwa walimu, hususan kutokana na kuchelewesha malipo na stahiki zao, kama vile posho za likizo, uhamisho na nyinginezo.
- Kutosimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyopitishwa kwenye vikao halali na kutothibiti makosa yanayobainika, kama vile ulevi, utoro wa walimu na wanafunzi.

b) **Mipango na Raslimali (Fedha za kuendesha na kusimamia mipango ya elimu)**

- Kukosekana kwa mikakati na mipango thabiti na endelevu ya maendeleo na kuinua taaluma na ufaulu. Ilibainika kuwa, mipango mingi iliyopo, ni ya zima moto, haina ushirikishaji makini na siyo endelevu.
- Ufinyu wa bajeti kutoka vyanzo vya serikali (Miongozo ya ukomo wa bajeti ya serikali ya kila mwaka inaathiri vinapumbele vya Halamshauri)
- Kukosekana vyanzo mbadala vya mapato nje ya ruzuku ya Elimu (*Capitation Grant*)
- Uwezo mdogo wa kiuchumi kwa wananchi na wazazi (Kushindwa kukidhi vipaumbele vya mahiaji ya familia).
- Kupungua kwa uwazi katika mapato na matumizi ya raslimali (Kupanga bajeti, kusimamia matumizi, kutoa taarifa sahihi na kwa wakati)

c) **Uwezo, weledi, ubunifu na umahiri katika ufundishaji na kujifunza**

- Upungufu wa walimu wenye umahiri kwenye baadhi ya masomo kama vile hisabati, fizikia, Kiingereza, ushauri-nasaha, nk.
- Ukosefu wa mafunzo rejea na endelevu kwa walimu wa masomo, walimu viongozi, kamati na bodi za shule,
- Kukosekana ubunifu na uthubutu wa kujaribu mbinu nje ya mfumo uliozoeleka (*Business as Usual*)
- Uelewa na mitazamo kinzani (*Mindset*) ya wazazi na jamii
- Kupungua kwa imani/matumaini ya wazazi kuhusu manufaa ya elimu. Hii ni pamoja na kukosekana kwa *role models* ndani ya familia na jamii.
- Tafsiri tofauti kwa baadhi ya sera za serikali hususan elimu bila malipo ya ada, kwamba ni elimu bure.

d) **Mwingiliano wa mamlaka za maamuzi ya kitaalamu na siasa**

- Baadhi ya viongozi wa kuchaguliwa ngazi za jamii, kama vile wenyeviti wa vijiji na madiwani, kuingilia utendaji wa shule na baadhi yao kukwamisha utekelezaji kwa makusudi na vitisho.

# 3.0 Mapendekezo na njia za kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kuinua ufaulu

## 3.1 Kuandaa na kutumia Ramani ya Mabadilliko (*Roadmap to Change*)

Washiriki wamebaini kuwa sehemu kubwa ya changamoto zilizopo zinaweza kutatuliwa na ziko kwenye uwezo wa wadau ndani ya jamii na shule. Washiriki walichambua na kutengeneza Ramani na njia ya Mabadiliko (*Roadmap to Change*) ya kila shule kwa kufuata vigezo vilivyotajwa hapo juu kama inavyooneshwa kwenye Kiamabatanisho No: 2. Jedwali hili la Ramani ya Njia ya Mabadiliko ya Elimu litatumika kwa kubainisha mambo ya kufanya na kuyawekea muda na kipaumbele katika muktadha wake. Maafisa elimu kata wataratibu ujazaji wa jedwali hili kwa ushirikiano na msaada kutoka kwa mtaalamu wa elimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## 3.2 Mapendekezo ya Hatua za Utekelezaji

| | Hoja ya pendekezo | Mhusika mkuu | Wahusika wasidizi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kwa kuwa madhaifu katika sekta ya elimu wilayani yanamuathiri mtoto wa Musoma, Wilaya ianzishe na kuendesha kampeni ya KOMBOA MTOTO NYANGETA NA ATHUMANI WAPATE ELIMU BORA | Mkuu wa Wilaya | Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Musoma |
| 2. | Kila shule iandae na kutekeleza ramani ya njia ya mabadiliko (*Roadmap to Change*) | Wakuu wa shule | Shule Kuu ya Elimu, Chuo kikuu cha Dar es salaam, |
| 3. | Wilaya iendeshe warsha za mafunzo ya uongozi kwa maafisa elimu kata, wakuu | Maafisa Elimu Wilaya (Elimu ya | • Maafisa Elimu Taaluma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa shule na walimu wa taaluma katika masuala ya<br>• Uongozi na utatuzi wa matatizo na migogoro,<br>• Usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji (mfano instructional supervision),<br>• Usimamizi na utekelezaji wa mipango, na mada nyinginezo | Msingi na Sekondari) | • Chuo Kikuu ch Dar es salaam na Ubunifu Assocites. |
| 4. | Kila shule iandae na kutekeleza mpango mahsusi ya Kutafuta vyanzo vya fedha na raslimali nyinginezo (*Resource Mobilization Strategy*) kwa maendeleo ya shule | Walimu wakuu na Kamati/Bodi za shule | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ubunifu Associates |
| 5. | Kwa kushirikiana na wadau, wilaya ianzishe na kuendeleza programu ya lazima na endelevu ya **LISHE na AFYA** kwa shule zote za msingi na sekondari | Walimu Wakuu na Viongozi wa Kamati/Bodi za shule | Global Community (Zamani PCI) |
| 6. | Kila shule itengeneze na kutekeleza Mpango Mkakati na Mipango Kazi ngazi ya shule. Kata pia ziwe na mpango wa elimu. | Wakuu wa shule. | Waratibu Elimu Kata<br>Shule Kuu ya Elimu, Chuo kikuu cha Dar es salaam na Ubunifu Associates |
| 7. | Kila shule ijenge na kuimarisha mahusiano, ushirikiano/ubia na taasisi mbalimbali za ndani na nje ili kuongeza maarifa ya kujifunza na ubunifu. | Walimu Wakuu, Kamati/Bodi za shule | Shule Kuu ya Elimu,Chuo kikuu cha Dar es salaam, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Mamlaka za uthibiti zimarishe ufuatuliaji na tathimini ya ufundishaji, ujifunzaji, na usimimizi wa mipango. | Kamati za uthibiti ubora ngazi ya shule | Ofisi ya Uthibiti Ubora Wilaya |
| 9. | Wilaya ianzishe na kuendesha program za mafunzo ya mbinu za ufundishaji zenye tija na ufanisI/weledi hususani katika masomo kwa kuanzia Hisabati, Fizikia Kiingereza, na jiografia | Kupitia MEWAKA | Shule Kuu ya Elimu, Chuo kikuu cha Dar es salaam na Idara ya Jiographia |
| 10. | Wilaya iendeleze juhudi za upatikanaji wa walimu wa kuajiriwa, tarajari, wanagenzi na wa kujitolea (waliofuzu mafunzo, wastaafu) na wa mazoezi kutoka katika vyuo vikuu na vyuo vya ualimu (kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa). | Afisa Elimu Wilaya | Shule Kuu ya Elimu, Chuo kikuu cha Dar es Salaam |
| 11. | Kila kata iandae na kutekeleza Mpango wa Ushirikishwaji wadau(*Stakeholder Engagement Plan*) ili kuimarisha taasisi zinazosaidia agenda ya elimu kama vile UWAWA, NGOs, Chama Cha Walimu Tanzania na asasi (NGOs) nyinginezo | Waratibu Elimu Kata | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,<br>Ofisi ya Maendeleo ya Jamii ya Wilaya |
| 12. | Kila shule ibuni na kuwekeza katika mikakati ya kuvutia watoto kupenda shule ( mfano, kuanzisha vilabu vya masomo, Michezo, Skauti, Kwaya, Matembezi ya kujifunza nje ya shule/kijiji, nk). | Walimu Wakuu, | Asasi za Kiraia, na Wawekezaji Sekta Binafsi |
| 13. | Viongozi wa siasa wafanye ziara za mara kwa mara shuleni kuongea na | Kila Diwani | Mkuu wa Wilaya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | walimu na wanafunzi kuhamasisha elimu bila kuingilia masuala ya kitaaluma na utendaji | | |
| 14. | Halmashauri iongeze kasi ya kushughulikia madai, stahiki, motisha endelevu kwa walimu na kutoa mrejesho. | AFISA ELIMU | TAMISEMI |
| 15. | Wilaya iendeleze majukwaa ya mijadala ya kila mwaka ili kupima mafanikio na kutafuta mbinu za kutatua changamoto za elimu kwa kadri zinavyojitokeza | AFISA ELIMU | Ofisi ya Mbunge |
| 16. | Mapendekezo yaliyotolewa katika mjadala huu yatumike kama Model ya kushughulikia ufumbuzi wa matatizo ya sekta ya elimu ya mkoa wa Mara na ikiwezekana nchi nzima | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Mbunge | Wasaidizi wa ofisi husika |
| 17. | Kuanzishwe mfuko maalum wa elimu wa Wilaya kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato kama vile marafiki wa Musoma Vijijini. Harambee mbalimbali za kutunisha mfuko wa elimu. Aidha, Halmshauri ya Musoma Vijini iangalie uwezekano wa kuanzisha tozo maalumu ya kuendeleza mfuko wa maendeleo ya elimu. Ili kuongeza mapato au vyanzo vya mapato ya katika ngazi za shule husika walimu wakuu wa shule wapewe mbinu za utafutaji wa vyanzo vya mapato kama vile kilimo cha bustani, ufujagaji wa kuku, nk. Halmashauri wa wilaya kwa | Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri, Ofisi ya Mbunge, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, | Wasaidizi wa ofisi husika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kushirikiana na wadau na marafiki wa Nyanja washirikiane kuwajengea uwezo wa *Fund Raising* na uandishi wa miradi itakayosaidia kupata fedhaa na misaada ya vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika maendeleo ya elimu ya jimbo la Musoma Vijijini. Jitihada zifanyike kuvisaidia vijiji vinavyostahili kupata mirahaba sahihi ya CSR kwa wakati kulingana na mikataba | | |
| 18. | Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Mbunge na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya waweke mikakati ya kuanzisha mashirikiano rasmi na taasisi zetu za Elimu ya Juu zilizopo ndani na Nje Ya Mkoa wa Mara. Ikiwezekana kufikia mwezi Juni, 2025 Halmashauri ya Musoma Vijijini iwe imesaini mkataba wa makubaliano na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Elimu itakayosaidia kwenye agenda ya maendeleo na Utawala wa Elimu na Idara ya Jiographia itakayosaidia kuimarisha ufundishaji wa somo la Jiographia, Utunzaji na Elimu ya Mazingira, Utatuzi wa migororo inayohusu rasilimali Pamoja na ardhi, Madiliko ya tabia ya nchi na matumizi bora ya ardhi na rasilimali zilizopo wilayani na Mkoa. Pia ikiwezkana | Ofisi ya Mkurugenzi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Mbunge na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Wasaidizi wa ofisi husika pamoja na wawakilishi wa ofisi husika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Serikali ya Wilaya /Mkoa iangalie uwezekano wa kuzishirikisha taasisi za binafsi zinazomilikiwa na wazawa wa Musoma vijijini/Mara ili kuongeza nguvu ya ushauri wa kitalaamu kwenye maswala mbalimbali ya maendeleo ya Elimu na Sekita zingine za maendeleo. Inapendekezwa pia Serikali ya Wilaya na Mkoa zishirikiane kuona uwezekano wa kushirikisha wilaya zingine za mkoa kushirikiana katika utekelezaji wa makubaliano haya ili kupunguza gharama utekelezaji wa makubaliano haya | | |
| 19. | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi , Ofisi ya Mbunge, Mwenyekiti wa Halmashauri washirikiane Kuanzisha na kuilea Taasisi ya Kijamii (NGO) ie Nyanja Develop Initiative itakayotumika kama chachu ya maendelo, mikakati na mipango mbadala wa kuleta suluhisho la matitizo mbalimbali kwenye jamii. Taasisi hii pia inaweza kusaidia kwenye utafutaji wa rasilimali fedha, uhamasishaji wa maendeleo, uanzishwaji na utekelezaji wa miradi mbalimbali nje ya mfumo maalumu wa serikali | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mbunge, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi | Watendaji na Wasaidizi wa ofisi husika |

## 4.0 Hitimisho na Maoni ya Wawezeshaji

### 4.1 Kupitia Washa washiriki wamepata kujifunza yafuatayo

i. Njia ya maendeleo ya ukweli inahitaji kujitoa na dhamira inayotoka moyoni. Ushirikiano wa viongozi na wadau ni nguzo imara katika katika kutatua changamoto kubwa na ndogo. Imedhihirika kuwa matatizo kadhaa yanayokwamisha maendeleo ya elimu hayahitaji pesa kuyatatua..

ii. Masuala yaliyoibuliwa yameongeza ufahamu na hamasa ya wadau wa elimu na imetengeneza dira ya utekelezaji (*Roadmap to Change*). Hata hivyo, kuna haja ya kukamilisha zoezi hili kiutafiti kwa uchambuzi wa kina wa *course and effect*, kutengeneza na kutekeleza model ya utatuzi na kufanya tathmini mbeleni.

### 4.2 Hitimisho na Mafunzo Makuu yaliyotokana na Mjadala:

Kupitia washa hii ya Uchambuzi, Utatatuzi na Uwajibikaji wa Pamoja Tumejifunza mambo yafutayo.

iii. Tumejifunza pia viongozi waliochaguliwa na wawakilishi wa wananchi na kiungo na kichocheo muhimu cha maendeleo ya elimu na sekta zingine. Ufanisi, uamminifu, uwezo wao wa kujitoa na ufatiliaji wa mambo ni muhmu sana kwenye kuleta maendeleo ya wananchi

iv. Mwitikio, hisia na mguso wa wadau ulionekana kupitia washa hii imedhihirisha kwamba sekita ya elimu itaendelea kuwa kitovu cha maendeleo ya sekita zingine na hivyo inahitaji kupewa umuhimu wa pekee katika mipango ya halmashauri na serikali ya wilaya

v. Kama zilivyo sehemu nyingine za dunia, nchi na mkoa matattizo yanayoikabili sekita ya elimu ya wilaya ya Musoma vijijini ni mtambuka na hivyo ufummbuzi wake unahitaji mbinu mtambuka

vi. Ushirikishwaji wa wadau hasa wazawa wa eneo husika ni kitu cha muhimu sana kwenye utafutaji wa suluhu za kudumu,nafuu na rahisi.Jitihada za makusudi na za haraka zifanyike li kuongeza ushiriki na kujitoa kwa wazawa kwenye mipango ya maendeleo ya wananchi kwenye maeneo walikozaliwa

vii. Tumejifunza pia kwamba matatizo mengi yanayoikabili sekita ya elimu wilaya ya Musoma vijijini siyo yote yanahitaji rasilimali fedha bali uwajibikaji thabiti na ushirikiano wa pamoja miongoni mwa wadau

viii. Sekita ya elimu Wilaya ya Musoma Vijijini inakabiliwa na mapungufu makubwa ya rasilimali (*Resource starvation*) na hivyo jitihada za haraka zinahitajika ili kupunguza pengo la rasilimali mbalimbali.

ix. Tumejifunza pia kwamba uongozi na utawala bora katika ngazi ya halamshauri, kata, vijiji na mashule inaweza kupunguza matatizo ya sekita ya elimu kwa zaidi ya asilimia arobaini.

x. Ufumbuzi wa matatizo ya Elimu lazima ufanywe kwa njia ya sahii. Methodolojia iliyotumika kwenye hii washa imewezesha kupata taarifa na majawabu(suluhisho) sahii la maendeleo ya sekita ya elimu wilaya ya Musoma Vijijini

xi. Ushirkiano na ushirkiano wa wadau na hasa viongozi katika ngazi ya wilaya na mkoa ni muhimu sana katika kupata ufumbuzi wa matatizo na maendeleo ya sekita elimu.

xii. Uwazi na ukweli na kujitoa kikamilifu ni nguzo muhimu ya kupata ushirikiano wa wadau mbalimbali

**4.3 Maoni ya timu ya wawezeshaji**

Kutokana na maoni na mapendekezo ya walengwa wa Washa, timu ya wataalamu inapependekeza kufanyika kwa mambo haya

i. Ni matumaini yetu kwamba hatua hii ya awali iliyofanyika kwa njia ya mjadala itaendelezwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha zoezi zima la kitafiti na taarifa ambazo zilikuwa zikiendelea kukusanywa toka kwa washiriki wa wa washa.

ii. Walimu waboreshewe mazingira ya kazi

iii. Ajenda ya kuimarisha mikakati ya ufaulu na maendeleo ya shule iwe ya kudumu na msukumo mkubwa.

iv. Tunapendekeza pia kwamba mambo ya kimaamuzi yasiyohitaji fedha yaliyojadiliwa na kupendekezwa kupitia mjadala huu yafanyiwe kazi kwa haraka ili kupunguza kadhia kwa wanaunzi na walimu.

v. Suala la kumairishwa kwa uongozi na utawala bora shuleni lifanyiwe kazi kwa haraka. Ikiwezekana walimu wakuu hasa wale ambao shule zao hazifanyi vizuri sana wawekewe malengo ya utendaji. Suala la Uteuzi wa viongozi wa mashule pia uzingatie weledi na uzoefu na panapobidi walimu/wakuu wawe wanabadilishiwa vituo vya kazi ili kuwapatia hali na kasi mpya ya kazi.

vi. Jukwaa kama hili lifanyike kila mwaka kama sehemu ya tathimini na kupata mrejesho wa yale yaliyojadiliwa na kuamuliwa .

vii. Jukwaa na miradi itakayotokanana na zoezi hili isambazwe (*Scaled Up*) katika ngazi ya Mkoa ili kuongeza matokeo chanya na kuwafikia watu wengi zaidi. Utekelezaji wake katika nagzi ya mkoa pia utaongeza nguvu ya kiutendaji hasa uungwaji mkono wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kiutawala na rasilimali zinazohitajika katika ngazi za utekelezaji. Tungetamani pia kuona matokeo, mapendekezo na Suluhu zilizotokana na mjadala huu zikiawa *scaled up* katika ngazi ya taifa kwa kadiri itakavyowezekana.

viii. Viongozi wa ngazi mbalimbali, yaani Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mbunge na Mwenyekiti wa Halmashauri washirikiane kufanya ushawishi wa mabadiliko ya kisera ili kuondoa baadhi ya vikwazo vinavyotokana na miongozo, sera na sheria ya elimu. Kwa mfano, pamoja na umuhimu na matokeo ya sera ya elimu bure, tafasiri yake ni kama vile haikueleweka vizuri kwa wadau hasa wazazi na jamii. Mkoa na Wilaya vinaweza kuomba mabadiliko kidogo ya hii sera ili wazazi wawe wanachangia pesa kidogo itakayosaidia kupunguza makali ya ukosefu wa mahitaji ya uendeshaji wa shule.

## Rejea


- MoEST (2023). BEST
- Mjadala wa Mkoa kuhusu Elimu 2019
- Mjadala wa Wakuu wa Sekondari Musoma DC 2021

# Viambatisho

**Kiambatisho A: Fomu ya Tathmini ya hali ya kila shule**

**HALI YA SHULE WILAYANI MUSOMA KWA VIGEZO**

Jina la Shule ______________________________________________

| Eneo | Kigezo | Alama jumla | Kigezo kidogo | Kiwango cha alama | Alama halisi | Ufumbuzi/Hatua ya kuchukua |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 Uongozi | Shule hii ina uongozi mahili na wenye weledi. | 10 | Maamuzi katika shule hii yanafanyika kwa usahihi na kwa namna ambayo inainua taaluma ya shule. | 2 | | |
| | | | Ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya kitaaluma unafanyika katika shule hii. | 2 | | |
| | | | Matatizo yote yanayojitokeza shuleni yanatatuliwa haraka na kwa usahihi hivyo kuleta tija katika maendeleo ya kitaaluma | 2 | | |
| | | | Ushirikishaji wa walimu, wanafunzi na wadau wengine katika shule hii ni wa kiwango cha juu | 2 | | |
| | | | Kuna uwajibikaji wa uongozi katika matokeo ambayo shule inayapata. | 2 | | |
| 2 Mipango | Shule hii ina mipango na inaitekeleza ipasavyo. | 10 | Shule hii ina dira na malengo ya ufaulu yanayotekelezeka kwa ajili ya maendeleo kitaaluma | 4 | | |
| | | | Shule hii ina utaratibu mzuri kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji na kufanya tathmini | 3 | | |
| | | | Shule hii ina mpango mkakati na mpango kazi wa kila mwaka unaotekelezeka | 3 | | |
| 3. Walimu | Shule ina walimu wenye vigezo na uwezo | 10 | Shule hii ina walimu waliokamilika kitaaluma. | 2 | | |
| | | | Walimu wa shule hii wana motisha wa hali ya juu ya kufanya kazi | 2 | | |
| | | | Shule ina mazingira mazuri ya walimu kufanya kazi | 2 | | |
| | | | Shule ina walimu wa kutosha wa masomo ya | 2 | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | hisabati na sayansi | | | |
| | | | Walimu wa shule hii wanapata mafunzo kazini mara kwa mara kwa ajili ya kuboresha utaalamu. | 2 | | |
| 4. Wanafunzi | Wanafunzi katika shule hii wana ari ya kujifunza | 10 | Wanafunzi katika shule hii wana morali wa kujifunza. | 2 | | |
| | | | Shule inatoa motisha kwa wanafunzi ili wafanikiwe kitaaluma | 2 | | |
| | | | Wanafunzi wana mazingira mazuri ya kujifunzia hapa shuleni. | 2 | | |
| | | | Tabia na mienendo ya wanafunzi katika shule hii ni ya kiwango kizuri | 2 | | |
| | | | Wanafunzi wanajifunza kwa ushirikiano miongoni mwao. | 2 | | |
| 5. Mazingira | Shule ina mazingira mazuri ya kujifunzia | 10 | Shule hii ina vichocheo chanya vya tabia za kujifunza | 2 | | |
| | | | Shule hii imejenga usawa kati ya wavulana na wasichana | 2 | | |
| | | | Shule hii imedhibiti uonevu kwa wanafunzi wote | 2 | | |
| | | | Shule hii haina unyanyapaa wa aina yoyote | 2 | | |
| | | | Mazingira ya kijiografia katika shule hii ni tulivu sana kiasi cha kuruhusu ujifunzaji vizuri | 2 | | |
| 6. Ufundishaji | Shule hii ina ufundishaji na ujifunzaji ni kamilifu | 10 | Katika shule hii ufundishaji unafanyika kwa ushirikiano baina ya uongozi na walimu (kuna clinical supervision) | 2 | | |
| | | | Katika shule hii kila somo linafundishwa kwa ukamilifu kwa kukamilisha muhitasari husika na kufanya upimaji wa ujifunzaji | 2 | | |
| | | | Katika shule hii mbinu za kisasa na zenye ufanishi ndizo zinazotumiwa na walimu katika kila somo | 2 | | |
| | | | Walimu wanawapatia wanafunzi mazoezi ya kutosha na wanawapa mrejesho unaowasaidia kufanya vizuri zaidi. | 2 | | |
| | | | Ufundishaji wa nadharia na vitendo ni kamilifu katika shule hii | 2 | | |
| 7. Mi | Shule hii ina vifaa miundombinu inayofanikisha maendeleo ya | 10 | Shule hii ina maktaba yenye vitabu vya masomo yote, vya kutosha na vinatumiwa | 2 | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | kitaaluma | | kikamilifu na wanafunzi kujifunza. | | | |
| | | | Shule hii ina mahabara za sayansi na kompyuta zenye vifaa vya kutosha na zinatumiwa kwa ukamilifu na wanafunzi katika masomo yao. | 2 | | |
| | | | Walimu wanapata na kutumia zana toshelevu za kufundishia na kujifunzia. | 2 | | |
| | | | Shule ina madarasha yenye viwango ya kutosha na yanayoendana na idadi ya wanafunzi | 1 | | |
| | | | Shule ina maji safi na salama | 1 | | |
| | | | Shule ina umeme wa uhakika | 1 | | |
| | | | Shule ina nyumba za walimu za kutosha na mabweni | 1 | | |
| 8. Huduma | Shule ina huduma wezeshi nzuri na toshelevu | 10 | Shule inawapatia wanafunzi chakula bora chenye virutubisho vinavyojenga uwezo wa kiakili na afya ya mwili. | 3 | | |
| | | | Shule inamtumia mshauri nasaha kuwapa ushauri wanafunzi katika masuala mbalimbali ya kimaisha. | 2 | | |
| | | | Shule inatoa ushauri mzuri wa kuwaelekeza wanafunzi kuhusu masomo yao na matarajio ya kazi za baadaye. | 3 | | |
| | | | Shule ina utaratibu mzuri wa huduma za kiafya na hususan zinazozingatia mahitaji ya wanafunzi wa kike. | 1 | | |
| | | | Shule ina huduma mabalimbali za burudani na michezo kwa ajili ya wanafunzi. | 1 | | |
| 9. Jamii | Uungwaji mkono kutoka kwenye jamii inayoizunguka shule ni mzuri. | 10 | Shule hii inazungukwa na jamii ya watu wanaopenda maendeleo ya kielimu | 2 | | |
| | | | Wananchi wanashiriki kikamilifu katika kazi za kuiendeleza shule hii. | 2 | | |
| | | | Jamii inafuatilia na kuiwajibisha shule kutokana na matokeo ya mitihani yanayopatikana hapa. | 2 | | |
| | | | Wazazi wanawapa ushirikiano wa kutosha walimu na wanafuatilia maendeleo ya watoto | 2 | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wao shuleni. | | | |
| | | | Watu wenye ushawishi, uwezo wa kifedha, na wenye mamlaka walioko ndani na nje ya Musoma wanashirikishwa kikamilifu katika kuiendeleza hii shule. | 2 | | |
| 10. Mamlaka za juu | Shule ina usaidizi wa karibu sana kutoka taasisi nyingine kupitia uongozi wa juu wa elimu na wataalamu. | 10 | Shule hii inashauriwa mara kwa mara na uongozi wa elimu katika kata | 2 | | |
| | | | Shule hii inapata ukaguzi wa kutosha na wenye msaada kutoka kwa wathibiti ubora wa karibu. | 2 | | |
| | | | Shule hii inapata usimamizi wenye manufaa kutoka kwa maafisa elimu wa wilaya na mkoa. | 2 | | |
| | | | Shule hii inapata usaidizi wa kutosha kutoka serikali ya kijiji, ofisi ya diwani na halmashauri ya wilaya. | 2 | | |
| | | | Shule hii inapata ushirikiano wenye manufaa kutoka taasisi za elimu ya juu na wataalamu mbalimbali wa elimu. | 2 | | |
| **TOTAL** | | **100** | | **100** | | |

**Kiambatisho B: Mfano wa Ramani ya Njia ya Mabadiliko katika Elimu Wilaya ya Musoma kwa kila shule**

**Shule** ___________________________________________

| Eneo | Kigezo Kidogo | Alama | Ufumbuzi | Kiashiria cha utendaji (KPI) | Shabaha | Muda | Rasilimali zinazohitajika | Chanzo na wadau | Ofisi ya kuwajibika | Ushahidi wa kuthibitisha | Umuhimu na uharaka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uongozi | Maamuzi katika shule hii yanafanyika kwa usahihi na kwa namna ambayo inainua taaluma ya shule. | 1 | Maamuzi wa kitaaluma shuleni yafanyike katika vikao rasmi vinavyoshirikisha walimu | Idadi ya Vikao | 6 | Dec 2025 | 600,000.00 | Ruzuku toka serikalini | mm | Mihutasari | JJ |
| | Ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya kitaaluma unafanyika katika shule hii. | 1 | Uongozi wa shule utayarishe na kutumia ubunifu mbalimbali kuendeleza taaluma shuleni | Idadi ya Vikao | 5 | Dec 2025 | 1,000,000.00 | Ruzuku | Mwal mluu | Motisha | JJ |
| | Matatizo yote yanayojitokeza shuleni yanatatuliwa haraka na kwa usahihi hivyo kuleta tija katika maendeleo ya kitaaluma | 0.5 | Uongozi wa shule ubaini na kutatua kwa wakati kila changamoto inayojitokeza shuleni. Viongozi wapate mafunzo kazini katika utatuzi wa matatizo. | Idadi ya Vikao | 3 | Dec 2025 | 4,000,000.00 | Ruzuku | Mwl Mkuu | Mihutasari | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ushirikishaji wa walimu, wanafunzi na wadau wengine katika shule hii ni wa kiwango cha juu | 1 | Shule ziongeze idadi ya wawakilishi wa walimu, wanafunzi na wadau katika kushughulikia masuala ya taaluma. | Idadi ya Club za masomo | 7 | Dec 2025 | 20,000.00 | Ruzuku | Mwal mkuu na mtaaluma | Vilabu masomo | JJ |
| | Kuna uwajibikaji wa uongozi katika matokeo ambayo shule inayapata. | 0.5 | Kila kiongozi na kila mwalimu awajibike kila matokeo ya mitihani yanapotoka yawe mazuri au mabaya kwa kuyatoela maelezo mbele ya wadau. | Idadi ya tathmini | 4 | Dec2025 | 50,000.00 | Ruzuku | Mwl mkuu | Mihutasari | JJ |
| Mipango | Shule hii ina dira na malengo ya ufaulu yanayotekelezeka kwa ajili ya maendeleo kitaaluma | 2 | Kila shule iweke malengo ya ufaulu ya kila mwaka na kuyatekeleza. | Idadi ya Mipango mikakati | 6 | Dec 2025 | 100,000.00 | Ruzuku | Mwl mkuu na Mtaaluma | Mihutasari | JJ |
| | Shule hii ina utaratibu mzuri kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji na kufanya tathmini | 1.5 | Uongozi wa shule, uthibiti ubora wa ndani na walimu mmoja mmoja uwe na mikakati ya wazi ya M&E | Idadi walimu walioajiriwa | 12 | Dec 2025 | 500,000.00 | Wadau, Ruzuku | Mwl mkuu na mtaaluma | Faili ya mdhibiti ubora na mihutasari | Jc |
| | Shule hii ina mpango mkakati na mpango kazi wa kila mwaka unaotekelezeka | 2 | Shule iandike na kutumia mpango mkakati wa miaka mitano na mpango-kazi wa kila mwaka. | Idadi ya Mpango kazi wa jumla ya mwaka | 2 | Dec 2025 | Vifaa | Ofisi ya Mbunge | Mwal mkuu | Nakala mpango kazi | JC |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | Shule hii ina walimu waliokamilika kitaaluma. | 1 | Uongozi wa shule ufuatilie kuajiriwa kwa walimu wa kutosha serikalini na kufuatilia wapangwe palipo na upungufu. | Idadi ya Barua | 15 | Dec 2025 | 300,000.00 | Wazazi na jamii | Mwal mkuu | Mihutasari | JJ |
| | Walimu wa shule hii wana motisha wa hali ya juu ya kufanya kazi | 1 | Shule iwe na mpango kamilifu na unaotekelezwa wa kumotisha kila mwalimu. | Idadi ya Wawajibikaji | 12 | Dec 2025 | 500,000.00 | Wadau wa shule | Mwl Mkuu | Mihutasari | JJ |
| | Shule ina mazingira mazuri ya walimu kufanya kazi | 1 | Uongozi uchambue na kubaini vikwazo vya kimazingira kwa walimu na kuvitafutia ufumbuzi. | Idadi ya walimu waliopokelewa | 3 | Dec 2025 | 200,000.00 | Ruzuku | Mwl mkuu | Mihutasari | JC |
| | Shule ina walimu wa kutosha wa masomo ya hisabati na sayansi | 1 | Uongozi wa shule kwa kushirikiana na afisa elimu kata, ufuatilie upatinakaji wa walimu wa sayansi na histabati. | Uwiano wa msawazo wa waalimu | 1:45 | Dec 2025 | 200,000.00 | Serikali | Mwl mkuu, DED na AEK | Mihutasari | JC |
| | Walimu wa shule hii wanapata mafunzo kazini mara kwa mara kwa ajili ya kuboresha utaalamu. | 1 | Shule iwe na mpango wa mafunzo ya walimu kazini. MEWAKA ifanyike kwa walimu wote angalau mara | Idadi ya vikao vya MEWAKA | 40 | Dec 2025 | 600,000.00 | Shule, Watu | Mwl mkuu na Mtaaluma | Mihutasari | JC |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | moja kwa mwezi. | | | | | | | | |
| Wanafunzi | Wanafunzi katika shule hii wana morali wa kujifunza. | 1 | Walimu wote washirikiane katika kuhamasisha kila mwanafunzi kujifunza kwa kumfikia mwanafunzi mmoja mmoja. | Idadi ya wanafunzi waliokiwa ktk kujifunza | 600 | Dec 2025 | 50,000.00 | E.K na ruzuku | Ofisi ya Taaluma | Mihutasari | JJ |
| | Shule inatoa motisha kwa wanafunzi ili wafanikiwe kitaaluma | 0.5 | Kwa kufuata ngazi za ufaulu, kila shule itoe zawadi, utambuzi, nk kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani ya ndani na ya kitaifa. | Uwepo wa file za matokeo | Wanafunzi 24 | Dec 2025 | 80,000.00 | E.K, Ruzuku | Ofisi ya Mhasibu | Mihutasari | JC |
| | Wanafunzi wana mazingira mazuri ya kujifunzia hapa shuleni. | 1 | Vikwazo vyote vya kijiografia na kisaikolojia, kama vile kelele karibu na shule viondolewe na kudhibitiwa. | Uwepo wa mazingira Tulivu | Mazingira bora kwa wanafunzi 600 | Dec2025 | 100,000.00 | E,K, Ruzuku | Mwl mkuu na ofisi ya ushauri na unasihi | Uwepo wa utulivu shuleni | JJ |
| | Tabia na mienendo ya wanafunzi katika shule hii ni ya kiwango kizuri | 1 | Uongozi na walimu watoe mafunzo ya nidhamu kwa kila mwanafunzi, ndani na nje ya darasa. | Uwepo wa nidhamu shuleni | Nidhamu kwa wanafunzi | Dec 2025 | Watu, vitu na fedha | | Mwl mkuu na Nidhamu | Daftari la adhabu | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanafunzi wanajifunza kwa ushirikiano miongoni mwao. | 0.5 | Shule iwawezeshe wanafunzi kufanya kazi za pamoja, kupitia kuunda club za masomo (kila somo), na kufanya kazi-mradi katika vikundi. | Uwepo wa wa club za masomo | Wanafunzi 300 | Dec 2025 | 50,000.00 | Watu, walimu na wanafunzi | Ofisi ya Mtaaluma na mwal mkuu | Daftari la klabu za masomo | JC |
| Mazingira | Shule hii ina vichocheo chanya vya tabia za kujifunza | 0.5 | Shule iwe na vifaa vyenye kuvutia wanafunzi kuvitumia kujifunza wenyewe. | Uwepo wa Maktaba na chumba cha Zana | 2 | Dec 2025 | E.K, na Ruzuku | DED, Tamisemi | Ofisi ya DED na Mwal mkuu | Uwepo wa zana | JJ |
| | Shule hii imejenga usawa kati ya wavulana na wasichana | 1.5 | Shule iwe na dawati la jinsia. | Vikao vya walimu wa unasihi | 4 | Dec2025 | Vifaa na muda | Wanafunzi, walimu | Mwl mkuu, kamati ya shule | mihutasari | JC |
| | Shule hii imedhibiti uonevu kwa wanafunzi wote | 1 | Sheria ndogo za shule ziwekwe wazi kwa wanafunzi wote na adhabu za kuzivunja vitangazwe wazi.<br>Shule iwe na mfumo salama wa kukusanya taarifa kutoka kwa wanafunzi kuhusu uonevu. | Uwepo wa mbao za matangazo | 10 | Dec 2025 | Wat, fedha na muda | Wanafunzi na walimu | Mwl mkuu na kamati ya shule | Sheria za shule | JC |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shule hii haina unyanyapaa wa aina yoyote | 1.5 | Shule iendeshe semina za mara kwa mara juu ya elimu jumuishi. | Uwepo wa semina | 2 | Dec 2025 | Watu na fedha | Mwl mkuu na mwl wa nidhamu | Mwal mkuu | mihutasari | JJ |
| | Mazingira ya kijiografia katika shule hii ni tulivu sana kiasi cha kuruhusu ujifunzaji vizuri | 1.5 | Masuala yote yanayoondoa utulivu shuleni yabainishwe na kuondolewa. | mambo yaliyobainishwa yanayoondoa utulivu | 3 | Dec 2025 | Watu na muda | Jamii na muda | Ofisi ya mtendaji na mwl mkuu | Barua | JC |
| Ufundishaji | Katika shule hii ufundishaji unafanyika kwa ushirikiano baina ya uongozi na walimu (kuna clinical supervision) | 1 | Shule iendeshe semina ya clinical supervision, na kila mwalimu afanyiwe clinical supervision angalu mara moja kwa mwezi. | Idadi ya Walimu waliofanyiwa clinical supervision kwa muhula | 6 | Octoba 2025 | Muda, fedha na watu | Ruzuku, AEK | AEK, Mwl mkuu na mtaaluma | Mihutasari<br>Ratiba ya ufundishaji | JJ |
| | Katika shule hii kila somo linafundishwa kwa ukamilifu kwa kukamilisha muhitasari husika na kufanya upimaji wa ujifunzaji | 1 | Kila mwalimu awe na mpango na kuutekeleza wa kufundisha mada zote bila kuruka mada hata moja. Kwa mada ngumu aombe msaada ndani na nje ya shule. | Walimu kuwa na maazimio ya masomo yao | 10 | Oktoba 2025 | Muda, fedha na watu | Ruzuku, AEK na wafadhili | Mwl mkuu, Mtaaluma na walimu | Maazimio, Shajara na mihutasari | JJ |
| | Katika shule hii mbinu za kisasa na zenye ufanishi ndizo zinazotumiwa na walimu katika kila somo | 0.5 | Walimu wote washiriki mafunzo kazini ya mbinu za kisasa na zenye ufanisi za masomo | Idadi ta Walimu walioshiriki MEWAKA | 10 | Dec 2025 | Ruzuku, E.K na Wafadhili | Muda, watu na fedha | Mwl mkuu, Mratibu MEWAKA,Walimu | Mihutasari ya MEWAKA | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wanayoyafundisha. | | | | | | | | |
| | Walimu wanawapatia wanafunzi mazoezi ya kutosha na wanawapa mrejesho unaowasaidia kufanya vizuri zaidi. | 1 | Kila mwalimu atumie mpango endelevu wa mazoezi ya somo lake. Mrejesho wa zoezi, jaribio, au mtihani utolewe kwa haraka/kwa wakati na uwe mrejesho unaomsaidia mwanafunzi kupiga hatua. | Jaribio kwa kila mwezi. -mitihani miwili kwa mwaka | 12 | Dec2025 | Muda Watu fedha | Ruzuku, AEK Wafadhili | Mwl mkuu Mtaaluma walimu | Benki ya maswali Matokeo ya mitihani | JJ |
| | Ufundishaji wa nadharia na vitendo ni kamilifu katika shule hii | 1 | Ufundishaji wa somo darasani ufanyike kwa vitendo zaidi na kufanya majaribio katika mahabara kuongezwe hadi angalau nusu ya vipindi vya somo husika. | Uwepo wa zana na vitendea kazi vya ufundishaji | 10 | Dec 2025 | 200,000.00 | Ruzuku E.K Wafadhili | Mwl mkuu Serikali | Uwepo wa mahabara na vifaa vyake | JJ |
| Miundombinu | Shule hii ina maktaba yenye vitabu vya masomo yote, vya kutosha na vinatumiwa kikamilifu na wanafunzi kujifunza. | 1 | Shule iwe na mwalimu wa maktaba, afungue maktaba kuhudumia wanafunzi na uongozi wa shule uhakikishe vitabu vya masomo yote vipo. | Chumba, Shubaka na vitabu | 1 | Dec 2025 | 200,000.00 | Serikali na wadu wa elimu | Jamii na serikali | Uwepo wa maktaba na vifaa vyake | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shule hii ina mahabara za sayansi na kompyuta zenye vifaa vya kutosha na zinatumiwa kwa ukamilifu na wanafunzi katika masomo yao. | 1 | Mahabara zikaguliwe kubaini vifaa vinavyokosekana kisha uongozi ushirikishe wadau vyote vinunuliwe. | Chumba cha maabara | 1 | Dec 2025 | Watu, fedha | Serikali na wadau | Jamii na serikali | Uwepo wa maabara | JJ |
| | Walimu wanapata na kutumia zana toshelevu za kufundishia na kujifunzia. | 1 | Mtaaluma awezeshe ufaraguzi wa zana na utunzaji wake ziweze kutumika tena na tena. | Uwepo wa zana na makuzi | 6 | Dec2025 | Watu na fedha | Serikali na wadau | Jamii na serikali | Uwepo wa zana | JJ |
| | Shule ina madarasha yenye viwango ya kutosha na yanayoendana na idadi ya wanafunzi | 0.5 | Uongozi wa shule uwasiliane na mamlaka za juu kuhusu mapungufu yaliyopo na uwaelimishe wadau namna ya kuchangia jitihada za uwepo wa madarasa ya kutosha. | Idadi ya Vyumba vya madarasa | 8 | Dec 2025 | Watu, fedha na muda | Serikali ,wadau na jamii | Jamii na serikali | Uwepo wa vyumba vya madarasa | JJ |
| | Shule ina maji safi na salama | 0.5 | Shule ivune maji ya mvua, ichimbe kisima, na iliyoko karibu na mfumo wa maji ya mamlaka za maji ziunganishwe. | Vyanzo vya maji | 4 | Dec 2025 | Serikali, muda na fedha | Serikali na wadau | Jamii na serikali | Bomba na matenki | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shule ina umeme wa uhakika | 0 | Shule iandike mradi wa kuunganisha umeme wa TANESCO au kufunga wa nishati ya jua kwa kubainisha manufaa ya kuwa na mradi huo. | Uwepo wa umeme | Matumizi ya umeme | Dec 2025 | Watu,. Fedha Na muda | Serikali na wadau | Serikali na jamii | Uwepo wa umeme | JJ |
| | Shule ina nyumba za walimu za kutosha na mabweni | 0.5 | Shule ishirikishe jumuiya wa wahitimu wa shule hii, wadau na jamii katika kujenga mabweni na nyumba. | Idadi ya Majengo yaliyojengwa na jumuiya | 4 | Dec 2025 | 8,000,000.00 | Jamii na serikali | Serikali na jamii | Vyumba na mabweni | JJ |
| Huduma | Shule inawapatia wanafunzi chakula bora chenye virutubisho vinavyojenga uwezo wa kiakili na afya ya mwili. | 1 | Shule iuishe na mpango endelevu wa chakula shuleni. | Uwepo wa Ratiba ya utoaji chakula | 1 | Dec 2025 | 1,000,000.00 | E.K Jamii Ruzuku | Ofisi ya mwl mkuu jamii | Stoki ya chakula | JJ |
| | Shule inamtumia mshauri nasaha kuwapa ushauri wanafunzi katika masuala mbalimbali ya kimaisha. | 1 | Shule iwe na mwalimu mnasihi na ofisi ya ushauri nasaha. | Uwepo wa mwl mnasihi na ofisi yake | 2 | Dec 2025 | 25,000,000.00 | Wafadhili na ruzuku toka serikalini | Mwl mkuu, wadau wa elimu, serikali | Uwepo wa mwl wa unasihi na chumba anachotumia | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shule inatoa ushauri mzuri wa kuwaelekeza wanafunzi kuhusu masomo yao na matarajio ya kazi za baadaye. | 0 | Kila mwalimu apangiwe kila mwaka wanafunzi wa kuwashauri kitaaluma na kikazi. | Uwepo wa ratiba | 4 | Dec 2025 | 20,000,00 0.00 | Wafadhi li, Serikali, Ruzuku toka serekali ni. | Mwl mkuu, Mwl unasihi, mkurugenzi | Uwepo wa ratiba | JC |
| | Shule ina utaratibu mzuri wa huduma za kiafya na hususan zinazozingatia mahitaji ya wanafunzi wa kike. | 0.5 | Shule iwe na chumba maalum cha huduma za mabinti na box la huduma ya kwanza na mawasiliano ya haraka na kituo cha afya cha karibu. | Uwepo wa chumba maalum u na boksi la huduma ya kwanza | 1 | Dec 2025 | 20,005,00 0.00 | Ruzuku toka serikalin i, walimu | Ofisi ya mkurugenzi, Mwl mkuu. | Sanduku la huduma ya kwanza na chumba maalumu . | JC |
| | Shule ina huduma mabalimbali za burudani na michezo kwa ajili ya wanafunzi. | 0.5 | Viwanja vya michezo na ratiba ya burudani na michezo iwepo na kutelekezwa kwa kusimamiwa na mwalimu wa michezo. | Viwanja vya michezo na ratiba ya michezo | 4 | Dec 2025 | 200,000.0 0 | Walimu, Ruzuku toka serikalin i. | Mwl mkuu | Ratiba ya michezo na Viwanja vya michezo. | JJ |
| Jamii | Shule hii inazungukwa na jamii ya watu wanaopenda maendeleo ya kielimu | 1 | Utengenezwe mpango shirikishi wa uelimishaji jamii na utelekezwe kila mwezi. | Vikao vya uelimish aji | 4 | Dec 2025 | Muda,fedh a na watu | Jamii na walimu | AEK,VEO na Shule | Mihutasa ri ya vikao | JJ |
| | Wananchi wanashiriki kikamilifu katika kazi za kuiendeleza shule hii. | 1 | Mpango wa uelimishaji jamii uhamasishe ushiriki wa raia katika kuendeleza shule. | Vikao | 4 | Dec 2025 | Muda, fedha na watu | Jamii na Walimu | AEK, VEO, WEO | Mihutasa ri ya vikao | JJ |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jamii inafuatilia na kuiwajibisha shule kutokana na matokeo ya mitihani yanayopatikana hapa. | 0 | Mpango wa uelimishaji jamii utekelezwe kwa kuujulisha umma nafasi na nguvu zao katika kuiwajibisha shule. | Semina za kielimu | 3 | Dec 2025 | Wataalamu wa elimu, muda na fedha | Jamii, wadau na walimu | DAO, S.L.O,Wataalamu elimu | Mihutasari | JC |
| | Wazazi wanawapa ushirikiano wa kutosha walimu na wanafuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni. | 0.5 | Shule iuishe na kutumia UWAWA ipasavyo kwa vikao vya mwanzo na mwisho wa muhula. | Uwepo wa UWAWA | 2 | Dec2025 | Watu, muda na fedha | Wanajamii, UWAWA na Mwl mkuu | AEK, UWAWA na Kamati ya shule | Mihutasari | JJ |
| | Watu wenye ushawishi, uwezo wa kifedha, na wenye mamlaka walioko ndani na nje ya Musoma wanashirikishwa kikamilifu katika kuiendeleza hii shule. | 1 | Shule ibaini wenye ushawishi, uwezo wa kifedha, na wenye mamlaka walioko ndani na nje ya Musoma na kuanzisha uhusiano/mawasiliano nao. | Uwepo wa mwaliko waWadau wa ndani na nje | 2 | Dec 2025 | Watu, muda na fedha | Jamii, mwal mkuu na wadau | Mwl mkuu na AEK | Mihutasari na Barua za mialiko | JJ |
| Mamlaka za juu | Shule hii inashauriwa mara kwa mara na uongozi wa elimu katika kata | 1 | Shule ijenge uhusiano wa karibu na ofisi za kata ikiwemo kumshirikisha afisa elimu kata katika mipango na mikakati ya shule. | Uwepo wa vikao vya Kila mara na uongozi wa serikali | 6 | Dec 2025 | Fedha, watu muda | Ruzuku Misaada toka kwa wadau | Serikali Mwl mkuu AEK | Mihutasari Mpango kazi wa shule | JJ |
| | Shule hii inapata ukaguzi wa | 1 | Shule iimarishe uthibiti ubora wa | Uwepo wa | 10 | Dec 2025 | 100,000.00 | Ruzuku E.K | Mwl mkuu na walimu | Mihutasari ya | JJ |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kutosha na wenye msaada kutoka kwa wathibiti ubora wa karibu. | | ndani kwa kuwatumia walimu. | ratiba ya Ukaguzi | | | | | | vikao vya ukaguzi | |
| | Shule hii inapata usimamizi wenye manufaa kutoka kwa maafisa elimu wa wilaya na mkoa. | 1 | Shule iimarishe mawasiliano na afisa elimu wa wilaya na mkoa. | Uwepo wa ratiba ya Ufatiliaji | 1 | Dec2025 | Watu Muda fedha | Ruzuku. E.K | Uongozi wa halmashauri na mkoa Mwl mkuu | Ratiba ya Ufatiliaji Mihutasari | JJ |
| | Shule hii inapata usaidizi wa kutosha kutoka serikali ya kijiji, ofisi ya diwani na halmashauri ya wilaya. | 1 | Shule ijenge ushirikishaji wa ofisi ya serikali ya kijiji, diwani na mkurugenzi wa halmashauri | Uwepo wa vikao | 2 | Dec 2025 | Watu Muda | Wadau wa elimu | VEO Diwani DEO | Mihutasari ya Vikao | JC |
| | Shule hii inapata ushirikiano wenye manufaa kutoka taasisi za elimu ya juu na wataalamu mbalimbali wa elimu. | 0 | Shule iingie makubaliano ya ushirikiano na chuo kikuu chenye kitivo/shule kuu ya elimu. | Vipeperushi toka chuo husika | 10 | Dec 2025 | 200,000.00 | Ruzuku toka serikalini | Mwl mkuu, Wahusika vyuo vikuu Ofisi ya DED | Mihutasari ya vikao vya makubaliano | JJ |
| JUMLA | | 44 % | | | | | | | | | |